01

Office of Chief Government Statistician

Police Headquarter Zanzibar

# OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR KWA MWEZI WA JANUARI 2023

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA JANUARI 2023

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA

Jumla ya matukio 173 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Januari, 2023. Jumla ya waathirika 173 kati ya hao, waathirika Wanawake ni 18 (asilimia 10.4), wanaume watatu (3) sawa na asilimia 1.7 na watoto ni 152 sawa na asilimia 87.9, miongoni mwa watoto wasichana walikuwa 119 (asilimia 78.3) na wavulana walikuwa 33 (asilimia 21.7).


Kielelezo 1.1 Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Januari 2023




Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar

Wilaya ya Magharibi "A" na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 47) sawa na asilimia 27.2 kwa kila wilaya, ikifuatia wilaya ya Mjini ambapo imeripotiwa matukio 34 (asilimia 19.7). Wilaya ya Micheweni na Mkoani zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote ambapo matukio matatu (3) sawa na asilimia 1.7 kwa kila wilaya.

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Januari 2023**




Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 12.3 kutoka matukio 154 kwa mwezi wa Disemba, 2022 hadi 173 mwezi wa Januari, 2023. Aidha, Wilaya ya Mjini iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Disemba 2022 (matukio 37) ambapo wilaya ya Magharibi "A" na Magharibi "B" zimeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Januari 2023 (matukio 47) kwa kila wilaya. wilaya ya Micheweni iliripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote matukio mawili (2) yaliripotiwa kwa mwezi wa Disemba 2022 ambapo wilaya ya Micheweni na Mkoani zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote matukio matatu (3) kwa kila wilaya yameripotiwa kwa mwezi wa Januari 2023.

Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Disemba 2022 na Mwezi wa Januari 2023

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 |
| Kaskazini 'A' | 9 | 8 | 6 | 5 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 9 | 10 | 7 | 6 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 |
| Kati | 8 | 5 | 3 | 4 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 4 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 37 | 34 | 13 | 19 | 7 | 3 | 2 | 0 | 2 | 1 | 3 | 2 | 10 | 9 |
| Magharibi 'A' | 25 | 47 | 9 | 13 | 2 | 2 | 1 | 10 | 3 | 5 | 2 | 5 | 8 | 12 |
| Magharibi 'B' | 34 | 47 | 21 | 23 | 5 | 7 | 1 | 2 | 0 | 4 | 1 | 5 | 6 | 6 |
| Wete | 9 | 5 | 5 | 2 | 3 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 3 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 7 | 6 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 1 | 3 | 0 | 0 |
| Mkoani | 8 | 3 | 3 | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **154** | **173** | **77** | **83** | **27** | **19** | **5** | **12** | **11** | **13** | **10** | **18** | **24** | **28** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Miongoni mwa wanawake 18 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa ni tisa (9), Kuingilia kinyume na maumbile ni wawili(2), shambulio la aibu walikuwa wanawake wawili (2) na shambulio walikuwa wanawake watano(5).

Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Januari 2022 na Januari 2023

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 |
| Kaskazini 'A' | 2 | 8 | 0 | 5 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 10 | 1 | 6 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Kati | 6 | 5 | 3 | 4 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 4 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 7 | 34 | 5 | 19 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 2 | 9 |
| Magharibi 'A' | 10 | 47 | 7 | 13 | 0 | 2 | 1 | 10 | 0 | 5 | 0 | 5 | 2 | 12 |
| Magharibi 'B' | 13 | 47 | 1 | 23 | 0 | 7 | 2 | 2 | 1 | 4 | 1 | 5 | 8 | 6 |
| Wete | 11 | 5 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 3 | 0 | 2 | 1 | 5 | 0 |
| Micheweni | 9 | 3 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 |
| Chake Chake | 3 | 7 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **65** | **173** | **25** | **83** | **1** | **19** | **7** | **12** | **5** | **13** | **7** | **18** | **20** | **28** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Miongoni mwa watoto 152 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 74, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 19, wasichana walioingilia kinyume na maumbile ni 10, Kutorosha walikuwa 13(wasichana 12 na mvulana 1), shambulio la aibu walikuwa 16 (wasichana 14 na wavulana (2)) na shambulio walikuwa 20 ambapo wasichana walikuwa 9 na wavulana walikuwa 11.

Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Januari 2023

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 7 | 4 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 7 | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 30 | 17 | 3 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 | 4 |
| Magharibi 'A' | 39 | 12 | 2 | 8 | 4 | 1 | 2 | 2 | 4 | 4 |
| Magharibi 'B' | 46 | 23 | 7 | 2 | 4 | 0 | 5 | 0 | 2 | 3 |
| Wete | 5 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 7 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **152** | **74** | **19** | **10** | **12** | **1** | **14** | **2** | **9** | **11** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Miongoni mwa wanawake 18 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa ni tisa (9), Kuingilia kinyume na maumbile ni wawili(2), shambulio la aibu walikuwa wanawake wawili (2) na shambulio walikuwa wanawake watano(5).

Jadweli 1.4a: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya, Januari 2023

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kati | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'A' | 5 | 1 | 2 | 0 | 1 | 1 |
| Magharibi 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **18** | **9** | **2** | **0** | **2** | **5** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Jadweli 1.4b: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya, Januari 2023

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Matukio | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **3** | **0** | **0** | **0** | **3** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Watoto wenye umri wa miaka 11-14 imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 59) sawa na asilimia 38.8 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 15-17 (matukio 54) sawa na asilimia 35.5. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17(matukio 32) sawa na asilimia 43.2 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Januari 2023

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 2 | 2 | | | 2 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 10 |
| 6-10 | | 9 | 7 | | | 2 | 0 | 0 | 0 | 5 | 4 | 2 | 29 |
| 11-14 | | 31 | 7 | | | 3 | 0 | 5 | 0 | 5 | 5 | 3 | 59 |
| 15-17 | | 32 | 3 | | | 3 | 1 | 7 | 0 | 2 | 2 | 4 | 54 |
| **Jumla** | | **74** | **19** | | | **10** | **1** | **12** | **2** | **14** | **11** | **9** | **152** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Januari, 2023 yameongezeka kwa asilimia 19.6 (matukio 152) ukilinganisha na mwezi wa Disemba, 2022 (matukio 130). Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15- 17 kwa mwezi uliopita yamepungua kwa asilimia 5.3 kutoka matukio 57 kwa mwezi Disemba 2022 hadi matukio 54 kwa mwezi wa Januari 2023.

Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Disemba 2022 na Januari 2023

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | | |
| | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 |
| 0-5 | 2 | 2 | 2 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 6 | 10 |
| 6-10 | 5 | 9 | 13 | 7 | 0 | 2 | 1 | 0 | 3 | 5 | 4 | 6 | 26 | 29 |
| 11-14 | 21 | 31 | 10 | 7 | 2 | 3 | 2 | 5 | 0 | 5 | 6 | 8 | 41 | 59 |
| 15-17 | 40 | 32 | 1 | 3 | 1 | 3 | 7 | 8 | 1 | 2 | 7 | 6 | 57 | 54 |
| **Jumla** | **68** | **74** | **26** | **19** | **3** | **10** | **11** | **13** | **5** | **16** | **17** | **20** | **130** | **152** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwa mwaka uliopita yameongezeka kutoka matukio 49 kwa mwezi wa Januari, 2022 hadi matukio 152 kwa mwezi wa Januari, 2023, ambapo idadi ya matukio katika umri wa miaka yote yameongezeka kwa mwezi wa Januari 2023.


Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Januari 2022 na Januari 2023

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Jan 2022 | Jumla Jan 2023 |
| | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | | |
| 0-5 | 2 | 2 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 3 | 4 | 0 | 0 | 5 | 10 |
| 6-10 | 3 | 9 | 1 | 7 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 6 | 7 | 29 |
| 11-14 | 6 | 31 | 0 | 7 | 2 | 3 | 4 | 5 | 0 | 5 | 3 | 8 | 15 | 59 |
| 15-17 | 12 | 32 | 0 | 3 | 1 | 3 | 1 | 8 | 1 | 2 | 7 | 6 | 22 | 54 |
| **Jumla** | **23** | **74** | **1** | **19** | **6** | **10** | **5** | **13** | **4** | **16** | **10** | **20** | **49** | **152** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Matukio mengi zaidi yanaonesha kutokea nyumbani kwa mtuhumiwa (matukio 74) sawa na asilimia 42.8 ukilinganisha na maeneo mengine yaliyotajwa.

Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea, Januari 2023




Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Matukio 167 kati ya matukio 173 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Polisi sawa na asilimia 96.5, tukio moja (1) lipo Ofisi ya Mashtaka sawa na asilimia 0.6, matukio matatu (3) yapo mahakamani sawa na asilimia 1.7 na matukio mawili (2) yamefungwa na polisi sawa na asilimia 1.2.


Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa, Januari 2023

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | Waathirika | | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mwanamme | Wanawake | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwahuru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | | Wasichana | Wavulana | | | | | | |
| Kubaka | 83 | | 9 | 74 | | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 80 |
| Kulawiti | 19 | 0 | | | 19 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 18 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 12 | | 2 | 10 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 |
| Kutorosha | 13 | 0 | 0 | 12 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 18 | 0 | 2 | 14 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 |
| Shambulio | 28 | 3 | 5 | 9 | 11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 28 |
| **Jumla** | **173** | **3** | **18** | **119** | **33** | **3** | **0** | **0** | **2** | **1** | **167** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Disemba 2022 ni 189 kati yao 173 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 91.5 na 16 walikua jirani sawa na asilimia 8.5.

Kielelezo 1.4: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia, Januari 2023




Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Kiambatanisho

Jadweli 1.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Januari 2023

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani kwa Muathirika | 5 | | 5 | | 2 | 2 | 1 | | 1 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 5 | 3 | 8 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 46 | | 46 | | 10 | 10 | 5 | | 5 | 5 | 1 | 6 | 2 | 0 | 2 | 1 | 4 | 5 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 11 | | 11 | | 0 | 0 | 3 | | 3 | 4 | 0 | 4 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu za kazi | 0 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 |
| Skuli/ Madrasa | 0 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 3 | | 3 | | 1 | 1 | 1 | | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) | 18 | | 18 | | 6 | 6 | 2 | | 2 | 2 | 0 | 2 | 8 | 2 | 10 | 7 | 7 | 14 |
| **Jumla** | **83** | | **83** | | **19** | **19** | **12** | | **12** | **12** | **1** | **13** | **16** | **2** | **18** | **14** | **14** | **28** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Jadweli 2.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Januari 2023

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 8 | 5 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 10 | 6 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kati | 5 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 4 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| Mjini | 34 | 19 | 3 | 0 | 1 | 2 | 9 |
| Magharibi 'A' | 47 | 13 | 2 | 10 | 5 | 5 | 12 |
| Magharibi 'B' | 47 | 23 | 7 | 2 | 4 | 5 | 6 |
| Wete | 5 | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Micheweni | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 7 | 3 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 |
| Mkoani | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **173** | **83** | **19** | **12** | **13** | **18** | **28** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwezi Disemba 2022 na Januari 2023

| Aina ya Matukio | Idadi ya Waathirika | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 | Dis 2022 | Jan 2023 |
| Kubaka | 77 | 83 | 9 | 9 | 68 | 74 | | | | |
| Kulawiti | 27 | 19 | | | | | 26 | 19 | 1 | 0 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 5 | 12 | 2 | 2 | 3 | 10 | | | | |
| Kutorosha | 11 | 13 | 0 | 0 | 11 | 12 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 10 | 18 | 5 | 2 | 4 | 14 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Shambulio | 24 | 28 | 7 | 5 | 7 | 9 | 10 | 11 | 0 | 3 |
| **Jumla** | **154** | **173** | **23** | **18** | **93** | **119** | **37** | **33** | **1** | **3** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar

Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwezi Januari 2022 na Januari 2023

| Aina ya Matukio | Idadi ya Waathirika | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 | Jan 2022 | Jan 2023 |
| Kubaka | 25 | 83 | 2 | 9 | 23 | 74 | | | | |
| Kulawiti | 1 | 19 | | | | | 1 | 19 | 0 | 0 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 7 | 12 | 1 | 2 | 6 | 10 | | | | |
| Kutorosha | 5 | 13 | 0 | 0 | 5 | 12 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 7 | 18 | 3 | 2 | 4 | 14 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Shambulio | 20 | 28 | 10 | 5 | 5 | 9 | 5 | 11 | 0 | 3 |
| **Jumla** | **65** | **173** | **16** | **18** | **43** | **119** | **6** | **33** | **0** | **3** |

Chanzo: Chuo cha Mafunzo - Zanzibar

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa, Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**


OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
Sanduku la Barua,2321, MMP, Zanzibar
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR
Sanduku la Barua, 237, MMP,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136